# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)

Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


***Unapojibu tafadhali taja:***
**Kumb Na: NBS/S.40/21/460**

**YALIYOJITOKEZA**

**Tarehe: 16 Januari, 2012**

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI DESEMBA, 2011

### Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 19.8

### Jedwali 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Desemba 2011 (Septemba 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Des-2010 | Nov - 2011 | Des - 2011 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 103.17 | 126.80 | 131.09 | 3.4 | 27.1 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 100.75 | 105.78 | 106.59 | 0.8 | 5.8 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 102.15 | 111.70 | 112.96 | 1.1 | 10.6 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 98.30 | 121.85 | 122.64 | 0.6 | 24.8 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 101.30 | 115.34 | 116.10 | 0.7 | 14.6 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 100.36 | 103.25 | 103.38 | 0.1 | 3.0 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 101.03 | 112.58 | 112.34 | -0.2 | 11.2 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 99.36 | 98.20 | 98.14 | -0.1 | -1.2 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 97.95 | 101.15 | 101.13 | 0.0 | 3.2 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 99.94 | 105.82 | 105.79 | 0.0 | 5.9 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 100.36 | 112.97 | 113.99 | 0.9 | 13.6 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 100.02 | 107.78 | 108.60 | 0.8 | 8.6 |
| | **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | **100.0** | **101.70** | **119.41** | **121.79** | **2.0** | **19.8** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 102.85 | 125.27 | 129.20 | 3.1 | 25.6 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 95.23 | 133.08 | 134.25 | 0.9 | 41.0 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 100.32 | 112.48 | 113.03 | 0.5 | 12.7 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 101.09 | 109.38 | 109.84 | 0.4 | 8.7 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa wa mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwezi Desemba 2011 umeongezeka hadi asilimia 19.8 ikilinganishwa na asilimia 19.2 kwa mwezi wa Novemba 2011. Kwa ujumla Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 121.79 kwa mwezi wa Desemba 2011 kutoka 101.70 kwa mwezi wa Desemba 2010. Vyakula na Vinywaji Baridi vimeongezeka hadi asilimia 27.1 mwezi wa Desemba 2011 kutoka asilimia 26.1 kwa mwezi wa Novemba 2011.

## Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula

Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limeongezeka hadi asilimia 25.6 kwa mwezi wa Desemba 2011 ikilinganishwa na asilimia 24.7 kwa mwezi wa Novemba 2011. Kasi ya ongezeko kwa bidhaa zisizo za vyakula imeongezeka hadi asilimia 12.7 kwa wa Desemba 2011 kutoka asilimia 12.6 kwa mwezi wa Novemba 2011.


## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa watunga sera.

Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Desemba 2011 umepungua kidogo hadi asilimia 8.7 kutoka asilimia 8.8 kwa mwezi wa Novemba 2011. Hata hivyo, mfumuko wa bei wa nishati umeongezeka hadi asilimia 41.0 kwa mwezi wa Desemba 2011 kutoka asilimia 39.2 kwa mwezi wa Novemba 2011.

## MWELEKEO WA MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KUTOKA JANUARI HADI DESEMBA, 2011

### KIELELEZO 1: MWELEKEO WA MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KUTOKA JANUARI HADI DESEMBA, 2011. (SEPTEMBA 2010 = 100)




Wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa, Mfumuko wa Bei wa Taifa, Mfumuko wa Bei wa bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula umekuwa na mwelekeo unaofanana wa kuongezeka kwa kila mwezi kuanzia Januari hadi Desemba, 2011. Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa umeongezeka kutoka asilimia 5.5 mwaka 2010 hadi asilimia 12.7 mwaka 2011; hili ni ongezeko la asilimia pointi 7.2. Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kila mwezi ulikuwa asilimia 1.4 kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2011.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 2.0

Mfumuko wa Bei wa mwezi Desemba 2011 umeongezeka kwa asilimia 2.0, Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 121.79 mwezi Desemba 2011 kutoka 119.41 mwezi Novemba 2011. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za

vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na mchele kwa asilimia 10.6, mikate kwa asilimia 2.4, vitafunwa kwa asilimia 1.9, nyama kwa asilimia 4.0, samaki kwa asilimia 2.4, maziwa kwa asilimia 4.0, mafuta ya kupikia kwa asilimia 3.2, limao kwa asilimia 6.2, karanga kwa asilimia 7.2, mbogamboga kwa asilimia 5.5 na asali kwa asilimia 3.1.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Desemba 2011

Tafsiri: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inapima badiliko la uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma mbalimbali za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania itaweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Bei za Taifa (Fahirisi) unaongezeka, thamani ya fedha hupungua.

Thamani ya shilingi 100 imepungua kutoka mwezi Septemba 2010 hadi kufikia Shilingi 82 na senti 11 mwezi Desemba 2011.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei




Kielelezo namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei; fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi cha miezi minne iliyopita (Desemba, 2010 to Machi, 2011) zikilinganisha na fahirisi zingine isipokuwa kwa mwezi Aprili mpaka Desemba 2011, kwa upande mwingine kundi la nishati na mafuta limekuwa na fahirisi za juu kuliko makundi mengine katika kipindi hicho. Kwa kipindi cha miezi 12, kundi la nishati na mafuta limeonyesha kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**